



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UCHUKUZI  
SHIRIKA LA RELI TANZANIA



Simu: 2133990  
Telegram: Railways  
Nukushi: 2133428

Ofisi ya Uhushiano  
S.L.P 76959  
Barabara ya Sokoine  
Dar es Salaam

**TAARIFA KWA UMMA**  
**UPOKEAJI WA VICHWA 3 VYA TRENI ZA UMEME NA MABEHEDA 27 YA ABIRIA**

Dar es Salaam, Tarehe 30 Disemba 2023

Shirika la Reli Tanzania limepokea vichwa vipyta vitatu (3) vya treni za umeme vilivyooundwa na kampuni ya Hyundai Rotem na mabeheda mapya 27 ya abiria yaliyoundwa na kampuni ya ‘*Sung Shin Rolling Stock Technology*’ (SSRST) kutoka nchini Korea Kusini.

Serikali kuitia Shirika la Reli Tanzania ilifanya manunuzi ya vichwa vipyta 17 na mabeheda mapya 59 ya abiria kwa ajili ya uendeshaji wa reli ya kiwango cha kimataifa – SGR. Mpaka sasa Shirika limepokea vichwa vya treni ya umeme vinne (4) kati ya 17 kutoka kampuni ya Hyundai Rotem na mabeheda 56 kati ya 59 kutoka kampuni ya ‘*Sung Shin Rolling Stock Technology*’ (SSRST) ya nchini Korea Kusini.

Mabeheda matatu (3) yaliyosalia yanatarajiwa kuwasili nchini Februari, 2024. Vichwa 13 vilivybaki vinatarajiwa kuwasili kwa awamu kama ifuatavyo, vichwa sita (6) vitawasili mwezi Machi na vichwa saba (7) vitawasili Aprili, 2024.

TRC itaanza kupokea Seti ya kwanza (1) kati ya Seti 10 za treni za Kisasa (EMU) mwezi Machi 2024 Mei seti 2, Juni seti 2, Julai seti 2, Septemba seti 2 na seti ya mwisho mwezi Oktoba 2024.

Vichwa vilivyopokelewa, kiutendaji vina mwendokasi wa kilomita 160 kwa saa. Mabeheda 27 katika madaraja ya Uchumi na Biashara. Daraja la biashara (Business class) ni mabeheda 13, kila behewa lina uwezo wa kubeba abiria 45 na mabeheda ya daraja la Uchumi (Economy class) ni 14, kila behewa lina uwezo wa kubeba abiria 78 kwa kuzingatia viwango vya kimataifa kumuwezesha abiria kusafiri kwa amani na salama.

Shirika la Reli Tanzania linaendelea kupokea kwa awamu vitendea kazi kwa ajili ya uendeshaji wa reli ya kiwango cha kimataifa (SGR). Zoezi la majoribio ya vitendea kazi linaendelea kwa mujibu wa mkataba ili kuhakikisha vinaendana na mifumo ya miundombinu iliyojengwa nchini kabla ya kuanza uendeshaji wa kibiashara.

Jamila Mbarouk  
Mkuu wa Kitengo cha Uhushiano